**Soma vifungu vifuatavyo. Vina nafasi 1 mpaka 15. Kwa kila nafasi, umepewa majibu manne hapo. Chagua jibu lifaalo zaidi kati ya yale uliyopewa**

Baada __1__ wakuu ___2___ kampuni ____3____ kumfuta ___4___, hesabu za pesa ___5___ alifaa kupewa ___6___, lakini mwishowe iligunduliwa ___7___ pesa alizokuwa ___8___ na kampuni zilikuwa ___9___ ___10___ angelipwa maana alikuwa bado hajamaliza kulipa motokaa yake.

| | | | |
|---|---|---|---|
| **1.** A. ya | B. wa | C. la | D. za |
| **2.** A. la | B. cha | C. za | D. wa |
| **3.** A. hizo | B. hivo | C. huo | D. hio |
| **4.** A. kasi | B. kalamu | C. kazi | D. gange |
| **5.** A. ambazo | B. ambayo | C. ambao | D. ambalo |
| **6.** A. zilifanywa | B. ilifanywa | C. yalifanywa | D. ulifanywa |
| **7.** A. kua | B. ati | C. kwamba | D. juu |
| **8.** A. akidaiwa | B. akidai | C. akidaia | D. akidailiwa |
| **9.** A. mwingi | B. nyingi | C. mengi | D. mingi |
| **10.** A. kuliko | B. kuziliko | C. kuiliko | D. kuwaliko |

Mazingira hujumuisha vile vitu vinavyomzunguka binadamu. Ama kweli, binadamu na mazingira yake ___11___ kwa njia mbalimbali. Hivi ni kusema kuwa, binadamu huyahitaji mazingira kufanya ___12___ zake. Vile vile, mazingira huhitaji binadamu ili ___13___. Kwa kusema hivi, ni ___14___ kuwa binadamu anapokosa kuyatunza mazingira, ___15___ makaa yeye mwenyewe.

| | | | |
|---|---|---|---|
| **11.** A. hutegemea | B. hutegemeza | C. hutegemeana | D. hutegemelewa |
| **12.** A. shughuli | B. mambo | C. shuguli | D. makazi |
| **13.** A. amtunze | B. ayatunze | C. akitunze | D. ajitunze |
| **14.** A. shaghalabaghala | B. wasiwasi | C. abadaan kataan | D. dhahiri shahiri |
| **15.** A. hujipalilia | B. hujipaliwa | C. hujipalia | D. hujipalika |

***Chagua jibu bora zaidi kwa maswali kutoka 16 – 30***

**16.** Urefu wa Karen ni mita moja ilhali Jane ana urefu wa sentimita mia moja. Kwa hivyo,

A. Karen ni mfupi kumliko Jane
B. Jane na Karen wanatoshana kwa urefu
C. Jane ni mfupi kuliko Karen
D. Karen na Jane hawana kimo

**17.** Chagua neno sahihi kukamilisha sentensi:
Majani ya mti ule __________ kwa sababu ya ukame.

A. yalipukutika
B. yalimwagika
C. yalianguka
D. yalidondoka

**18.** Tulifika shuleni kabla ya wakati uliopangwa. Hii inamaanisha kuwa

A. tuliwai
B. tulikawia
C. tuliwahi
D. tulichelewa

**19.** Neno 'Alhamdulilahi' ni mfano wa

A. kiulizi
B. kiunganishi
C. kihusishi
D. Kihisishi

**20.** Wakati baada ya majogoo pia huitwa

A. machweo
B. macheo
C. machwa
D. magharibi

**21.** Kamilisha methali ifuatayo:
Mwenda tezi na omo

A. hana aendako
B. marejeo ni ngamani
C. huvikwa pete
D. huishia ukingoni

**22.** 3, 7, 17, 31 and 43 ni baadhi ya nambari

A. chanja
B. shufwa
C. witiri
D. tasa

**23.** Chagua jibu sahihi:
Wageni wote waliingia ___________

A. kwenye nyumbani
B. katika nyumba
C. kwa nyumba
D. nyumba

**24.** Jaza pengo kwa kutumia kiashiria radidi kifaacho
Vyombo _____ vitatumiwa na wageni hawa

A. hivi hivi
B. vivi hivi
C. zizi hizi
D. hivi vivi

**25.** Jaza nafasi kwa usahihi.
Msalihina ni mtu _________ ilhali ______ ni mtu mwenye baraka au aliyebarikiwa.

A. anayesalimu/barakao
B. anasali/bakari
C. anayesalimika/mubaraka
D. anayesali/mabruki

**26.** Umbo la mpira wa kandanda laweza kuelezwa kuwa ni

A. mviringo

B. mche

C. tufe

D. duara dufu

**27.** Tulianza safari jua likiaga miti. Ni kusema tulianza safari

A. jioni

B. asubuhi

C. adhuhuri

D. alfajiri

**28.** Chagua kundi la maneno ambayo ni vitenzi

A. Kasha, mwizi, jangili, mbeni

B. Mweupe, mrembo, mdogo, laini

C. Lima, funga, aga, koroma

D. Vizuri, polepole, vibaya, haraka

**29.** Mtamba huzaa ndama, akiwa wa kike huitwa _____ naye wa kiume huitwa _____

A. fahali/dachia

B. beberu/senge

C. mfarika/tembe

D. mori/njeku

**30.** Tarakimu 4,037,957 kwa maneno ni

A. milioni nne, sufuri thelathini na saba elfu, mia tisa na hamsini na saba

B. milioni nne, thelathini na saba elfu, mia tisa na hamsini na saba

C. nne milioni, laki thelathini na saba, mia sita na hamsini na saba

D. nne milioni, tatu na saba elfu, tisa tano saba

***Soma taarifa ifuatayo kisha ujibu maswali 31 mpaka 40***

Siku moja, Juma aliamua kwenda kuvua, kabla ya mafungulia ng'ombe. Kwa kuwa kulikuwa na baridi, aliamua kuvua shati lake na kuvaa koti la kahawia. Akachukua mshipi, ndoana na chambo kisha akaingia mtumbwini na kuelekea kwenye maji marefu. Akaanza kuvua. Mara mshipi wake ukaanza kuchezacheza, dalili kwamba ndoana yake ilikuwa imenasa samaki. Samaki mwenyewe alikuwa mkubwa sana. Ilimlazimu kupigana naye kwa muda mrefu sana kabla ya kumvua. Samaki mwenyewe alikuwa papa upanga.

Hakupoteza wakati kurudi ufuoni baada ya kumvua huyo samaki. Kufika ufuoni alishika kisu chake na kuanza kumchinja huyo samaki. Lo! Si maajabu aliyoyaona! Mara tu baada ya papa huyo kukatika vipande viwili, kichwa cha binadamu kisicho na kiwiliwili kilionekana ndani ya tumbo la huyu papa upanga. Juma hakupoteza wakati hata kidogo. Alitoka mbio na kuelekea kituoni alipopiga ripoti ya yale mambo aliyoyashuhudia. Polisi nao hawakupoteza wakati kwenda naye kwani siku mbili kabla ya siku hiyo ya Ijumaa wavuvi wawili walikuwa wamepotea majini kutokana na mtumbwi wao kuchukuliwa na upepo mkali sana.

**31.** Kulingana na aya ya kwanza, kazi aliyoamua kwenda kufanya Juma ni

A. kufua shati

B. kulisha ng'ombe

C. kuvua samaki

D. kuwinda wanyama

**32.** Maji marefu, kwa mujibu wa kifungu ni

A. maji yenye upana mkubwa

B. maji yenye kina kikubwa

C. maji yenye kimo kikubwa

D. maji yasiyokwisha upepo

**33.** Ishara ya kunasa samaki ni
A. mshipi kuchezacheza
B. ndoana kuchezacheza
C. mtumbwi kuchezacheza
D. mkono wa Juma kutikisatikisa

**34.** Samaki aliyevuliwa alikuwa wa
A. maji ya mtoni
B. maji ya bahari
C. maji ya chumvi
D. maji ya ziwani

**35.** Ni nini kinachoonyesha ukubwa wa samaki aliyevuliwa?
A. Upanga wa samaki
B. Tumbo lake huyo papa
C. Kichwa cha mtu kupatikana tumboni mwake
D. Juma kwenda kituoni kupiga ripoti

**36.** Maneno 'Kabla ya mafungulia ng'ombe,' yanarejelea wakati gani?
A. Alfajiri
B. Alasiri
C. Adhuhuri
D. Jioni

**37.** Madhumuni ya Juma kuenda kituoni yalikuwa ni
A. kuwajulia polisi hali
B. kuomba usaidizi kwa wavuvi waliopotea
C. kupiga ripoti kuhusu yale aliyoyaona
D. kuripoti kuhusu mtumwi wake uliopotea

**38.** Kiwiliwili ni
A. kichwa kilicho na mwili
B. mwili usio na kichwa
C. mzoga wa mnyama mwenye kichwa
D. mzoga wa mnyama asiye na kichwa

**39.** Neno jingine lenye maana sawa na kahawia ni
A. hudhurungi
B. buluu
C. manjano
D. samawati

**40.** Nini kisingemfanya Juma kwenda uvuvini tena?
A. Kule kushuhudia kichwa cha binadamu tumboni mwa papa
B. Kusikia amepoteza marafiki wawili
C. Kule kumwua papa mwenye upanga
D. Kule kupigana na samaki mkubwa

***Soma ufahamu ufuatao kisha ujibu maswali 41 mpaka 50***

Hayawi hayawi huwa. Awali, tulidhani ni mzaha. Kumbe mzaha hutunga usaha.

Mnamo mwezi wa saba mwaka jana muhula wa pili, mwalimu wetu wa Kiswahili alitutangazia kwenye gwaride kwamba tungefunga safari ya kwenda kutalii nchini Tanzania. Ziara hii iliandaliwa maalum na rasmi kwa ajili ya kuwaburudisha wapenzi wa wanachama wa Kiswahili wa shule yetu.

Mimi nilikuwa mwanachama wa mstari wa mbele. Licha ya hivyo nilikuwa nimeshikilia wadhifa wa ukatibu katika chama. Nilijua dhahiri shahiri kwamba chama chetu kingeenda safari hiyo.

"Safari hii tutafanya ziara kubwa kuliko ya mwaka jana," mlezi wa chama alianza. "Tutaanzia Mlima Kilimanjaro, tulale Arusha mjini. Kesho yake tuondoke kuelekea ziwa Manyara. Tutalale Mto wa Mbu. Baadaye tupasue milima na mabonde, misitu na nyika hadi tufike mbuga kuu ya Serengeti ambayo ni hifadhi maarufu ya wanyama katika ulimwengu mzima.

Kabla ya kuwasili Serengeti, tutapitia kituo cha historia cha Olduvai. Tutakuwa tukilala Seronera huku tukizuru mbuga ya Serengeti. Tutafika kilele cha ziara yetu kwa kutumbukia ndani ya

Ngorongoro kreta.

Licha ya joto jingi la Dar-es-salaam tulifurahi, tuliburudika na kufarijika hadi kikomo cha ziara yetu. Hiyo ndiyo ziara yetu kubwa iliyoandaliwa kwa muda wa miezi mitano. Mungu amsaidiae mwalimu wetu wa Kiswahili atuandalie ziara nyingine kama hiyo.

**41.** Kwa nini awali msemaji na wenzake waliona mambo kuwa ya mzaha?
A. Hawakuamini yangefanikiwa
B. Mambo yalianza mapema
C. Maandalizi yalikuwa duni
D. Mwalimu alitangaza gwarideni

**42.** Unafikiri ziara hii ilifanywa lini?
A. Muhula wa pili wakati wa likizo
B. Kwenye likizo ya mwisho wa mwaka
C. Katikati ya muhula wa kwanza
D. Kwenye muhula wa pili

**43.** Madhumuni makubwa hasa ya kufanywa ziara hii yalikuwa ni
A. kuwaburudisha na kuwafurahisha wanachama wa Kiswahili
B. kutembelea nchi ya Tanzania
C. kwenda kujifunza Kiswahili nchini Tanzania
D. kutembelea hifadhi ya wanyama Tanzania

**44.** Kabla ya kuingia mbugani Serengeti, watalii hawa walipitia
A. Manyara na Ngorongoro
B. Arusha na Karatu
C. Manyara na Genge la Olduvai
D. Seronera na Olduvai

**45.** Mahali palipovutia zaidi katika ziara hii ni
A. Arusha
B. Serengeti
C. Dar-es-salaam
D. Ngorongoro kreta

**46.** Mwandishi alishikilia wadhifa upi katika chama?
A. Alikuwa mwalimu wa Kiswahili
B. Alikuwa kiongozi mkuu
C. Alikuwa katibu
D. Alikuwa mweka hazina

**47.** Kreta iliyotajwa inaitwa
A. Ngorongoro
B. Dar-es-salaam
C. Olduvai
D. Arusha

**48.** Ziara ilipangwa na kuandaliwa na
A. mwalimu mkuu
B. katibu wa chama
C. wazazi
D. mwalimu wa Kiswahili

**49.** Bila shaka, wageni hawa walishuhudia mandhari gani ya Dar-es-salaam?
A. Milima mirefu
B. Mawingu mazito
C. Bahari na minazi
D. Joto jingi

**50.** Wito mkuu unaotolewa katika taarifa hii ni
A. Mungu amsaidie mwalimu wa Kiswahili
B. Tusome Kiswahili
C. Tuandaliwe ziara nyingine
D. Tuwe wanachama wa Kiswahili